

# Jinsi Nilivyobatizwa



**Habari! Mimi ni Ara-noarii. Ninaishi Tahiti. Mimi nina umri wa miaka 11, na ninahisi fahari kusema kumba mimi ni muumi-ni wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.**



## Ni kwa jinsi gani ulijifunza kuhusu Kanisa?

Marafiki fulani walialika familia yangu kwenye shughuli ya Kanisa. Sisi pia tulialikwa kwenye ubatizo wa mtoto. Nilimuuliza mama yangu kama ningeweza kukutana na wamisionari kwa sababu kweli nilitaka kujifunza zaidi kuhusu Yesu Kristo.



PICHA NA STEPHANE SAYEB

## Ilikuwa je kukutana na wamisionari?

Wamisionari walikuwa wakarimu kweli! Mimi daima nilisisimka kuwa na masomo na wao kumhusu Yesu Kristo na injili Yake. Nilipendelea hadithi walizonisimulia na michezo tuliocheza ili inisaidie kujifunza.



## Ubatizo wako ulikuwa je?

Baba yangu alimbatiza mama yangu pamoja na mimi kwenye siku yangu ya kutimiza miaka 11 ya kuzaliwa. Nilikuwa mwenye furaha sana! Tuliwaalika watu wengi ambaeo tunawapenda. Wanafunzi wenzangu na mwalimu walikuja kuniunga mkono.

Nilipotoka majini, nilijawa na shangwe. Nilitabasamu kabisa! Nilikuwa na furaha sana kwamba niliweza kufuata mfano wa Yesu Kristo.

## Je, ilikuwa kuwa kwenye darasa la Msingi kwa mara ya kwanza?

Mwanzoni, nilikuwa na wasiwasi nilikuwa karibu kulia. Lakini kisha nilienda kwenye shughuli ya Msingi. Nilipata kumjua kila mtu, na nikapata marafiki kadhaa.

Kama wewe ni mgeni, ushauri wangu ni njoo kwenye darasa lako la Msingi, hata kama unaogopa mwanzoni. Tunawapenda wageni!

## Je, ni kwa jinsi gani wewe unamfuata Yesu?

Ninasali na kwenda kanisani kila Jumapili. Ninazungumza na familia yangu kuhusu injili ya Yesu Kristo.

Ninajaribu kuwajali wengine ambaeo wanahitaji msaada. Nyumbani, ninamsaidia mama yangu kazi za nyumbani. Ninamsaidia baba yangu kazi za shamba, kukata kuni, na kujenga vitu. Miezi michache iliyopita kata yetu ilikuwa na maonyesho ya vippaji. Mimi ni mwanamuziki, kwa hiyo nilipiga ngoma usiku mzima!

**Ni nini kilikuwa kitu chako pendwa kuhusu kubatizwa? Au ni nini unategemea zaidi?**